



FAHARI YETU

HALMASHAURI YA ARUSHA

Arusha Dc Kazi Inaendelea



MRADI WA UPANUZI WA MIUNDOMBINU ZAHANATI YA MWANDET KUWA KITUO CHA AFYA



Milioni
590

HALIUZWI



www.arushadc.go.tz



Arusha District Council arusha_district_council

KUHUSU MRADI

Na Elinipa Lupembe

Serikali ya awamu ya sita, inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuboresha huduma za afya nchini kwa kusogeza huduma karibu na wananchi lengo likiwa ni kuondoa vifo vya kina mama na watoto wakati wa kujifungua.

Kufuatia mkakati huo Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 590 kwa ajili ya upanuzi wa zahanati ya Mwandeti kuwa Kituo cha Afya, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wanachi waishio maeneo ya pembezoni.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Selema Msumi, ameweka wazi kuwa kiasi hicho cha fedha kimetumika kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo pacha la mama na mtoto na upasuaji (maternity ward & theater), jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la kufulia pamoja na nyumba ya watumishi ya kuishi familia tatu (3 in 1).

"Katika fedha hizi, shilingi milioni 500 ni fedha za tozo ya miamala ya simu, na milioni 90 ni fedha za mapambano dhidi UVIKO 19, na tayari nyumba ya watumishi imekamilika na wameanza kuishi kwenye nyumba hiyo". Amesisistiza Msumi.

Nao wananchi wa Kata ya Mwandeti wameendelea kuishukuru Serikali ya awamu ya sita, kwa kuwapa fedha za ujenzi wa kituo cha afya, huduma ambazo

hapo awali walitembea umbali mrefu kuzifuata huku wakitumia gharama kubwa za matibabu na usafiri hasa wakati wa usiku.

Diwani wa kata ya Mwandeti Mhe. Logolie Lukumay, amesema kuwa, uwepo wa kituo cha afya Mwandet kitasaidia wananchi ambao waliteseka kutafuta huduma za afya kwa gharama kubwa na wengine kupoteza maisha kwa kukosa huduma za haraka.

Naye Mganga Mfawidhi Zahanati ya Mwandeti, Dkt. Aidan Martine amesema kuwa, uwepo wa nyumba za watumishi katika eneo la kazi, utawaongezea ari ya kufanya kazi na weledi katika kutekeleza majukumu yao, ikiwa ni pamoja na utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wagonjwa kwa urahisi na kwa haraka kwa muda wote wa siku.

"Daktari na wauguzi waishipo ndani ya eneo la kazi, inawarahisishia utekelezaji wa majukumu yao ya kazi, kuingia kazini kwa wakati, kutoa huduma kwa haraka hususani huduma za 'emergency' hasa wakati wa usiku, lakini pia inaongeza wigo kwa wagonjwa kupata huduma kwa saa 24" Dkt. Martine.

Zahanati ya Mwandeti iko umbali wa zaidi ya Km 47 kutoka makao makuu ya halmashauri, eneo ambalo wananchi wake waliteseka kwa muda mrefu kwa kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya jambo ambalo lilipelekea baadhi ya watu kupoteza maisha kwa kukosa ama kupata huduma kwa kuchelewa.



JENGO LA WAGONJWA WA NJE (OPD)



JENGO LA MAABARA (LABORATORY)



JENGO LA MIONZI (X-RAY)



JENGO LA MAMA NA MTOTO(MARTENITY WARD)



JENGO LA KUFULIA (LAUNDRY)




NYUMBA YA MTUMISHI (3 in 1)





FAHARI YETU

HALMASHAURI YA ARUSHA



enaboishu
FM RADIO 101.3

Mawasiliano; S. L. P 2330, Arusha | Barua pepe : ded@arushadc.go.tz


Fuatilia kurasa zetu za Mitando ya kijamii kwa habari na matukio mbalimbali zinazoenesha utekelezaji wa shughuli za Maendeleo katika Halmashauri ya Arusha kama zilivyoainishwa hapa chini.



www.arushadc.go.tz



Arusha District Council



[@arusha_district_council](https://www.instagram.com/arusha_district_council)